

Pambazuko

Toleo Namba 0049

Jumatatu Oktoba 1-8, 2023



**Mume nambari wahedi
yuko wapi?**

Uk. 5

NSSF yaja kivingine kuondoa umasikini

● *Machinga kuhusishwa zaidi*



Uk. 14

Utu umemtangulia Rugambwa, asema Askofu Bagonza



Uk. 6

**Kula
hovyoy,
kunaua
haraka**

Uk. 7

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri, Tangazo

Haya yatuepushe magonjwa ya moyo

KATIKA ukurasa wa saba wa gazeti hili kuna habari inayoeleza kuwepo kwa kasi ya ongezeko la wagonjwa wa moyo na shinikizo la damu kwa Watanzania.

Habari hiyo inaeleza kwamba Watanzania karibu milioni nne sasa, wanakabiliwa na matatizo ya afya ya moyo kutokana na kuendelea “kung’ang’ania mitindo ya maisha inayochochea ongezeko la idadi ya wagonjwa.

Takwimu za Wizara ya Afya Tanzania za mwaka 2022 zinaonesha kuwepo kwa ongezeko la asilimia 9.4 kwa wagonjwa wa moyo na shinikizo la damu.

Kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita; Tanzania imerekodi wagonjwa wa magonjwa hayo kutoka milioni 2.5 mwaka 2017 hadi wagonjwa 3.4 mwaka 2022.

Hakika takwimu hizo zinatisha na zinatoa angalizo kwamba kunahitajika hatua za haraka kukabili ongezeko hilo la wagonjwa wa moyo.

Sisi katika Pambazuko tunaamini kwamba magonjwa mengi ya moyo yanaweza kuepukwa ikiwa wananchi watazingatia ushauri wa wataalamu, hasa wale mabingwa wa magonjwa ya moyo.

Kwamba endapo watu wataamua kuacha matumizi makubwa ya kula chumvi nyingi, kuacha kula mafuta mengi na kuacha kufakamia vyakula vya sukari nyingi, ushindi wa magonjwa hayo ni uhakika.

Pia ili kuhakikisha magonjwa ya moyo yanatokomezwa, ni vyema wananchi wakazingatia ulaji wa mboga-mboga nyingi, matunda na kufanya mazoezi zaidi.

Tunaweza.

Changia kuwezesha Pambazuko

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufurahia kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakitumia fedha, muda, ujuzi na rasirimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Bado uongozi wa Pambazuko haukubaliani na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hili kuanza kuuzwa kwa umma.

Lakini, uongozi umekubaliana na mawazo ya kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapenda kuchangia

maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chohote kinapokelewa kwa shukrani.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu ya mkononi – kupitia namba hii ya TiGO; 6014500

Pia unaweza kuskani “QR Code hiyo na utoingia kwenye utaratibu wa kuanza kutuma mchango wako.

Tunaahidi kwamba kwa mchango wako, gazeti la Pambazuko litakuwa bora zaidi na kuendelea kukufikia wewe pamoja na umma wote BURE.

Kwa maelezo zaidi wasiliana kwa namba hii: 0744 768 263.

Mhariri Mkuu, Oktoba, 2023

POLEPOLE TUTAFIKA...



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe (kushoto), akimsikiliza Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe walipokutana Unguja, Zanzibar wiki iliyopita. Viongozi hao pamoja na wakuu wengine wa vyama vya siasa, walikutana kujadili masuala mbalimbali ya siasa, ikiwamo maandalizi ya uchaguzi mkuu na mchakato wa kupatikana Katiba mpya. (Picha kutoka akaunti ya X ya Zitto Kabwe).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Utukufu mkubwa katika maisha siyo katika kuanguka kamwe na kukata tamaa, lakini kwa kuamua kunyanyuka na kusonga mbele kila tunapoanguka – Nelson Mandela (Rais wa Afrika Kusini huru isiyokuwa ya ubaguzi).

Uchambuzi

Z'Bar yazinduka kulinda mazingira

Na Jabir IDRISSE,
Zanzibar

HATUA ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuanzisha utaratibu wa kutunga Sera ya Mazingira inayozingatia hali halisi ya zama hizi, ni ya kuungwa mkono.

Ni hatua ya kuungwa mkono na umma pamoja na wadau wa nje wakiwemo washirika wa maendeleo ambao wana jukumu muhimu la kusaidia nchi zinazoendelea kujenga uwezo wa kuhimili athari za kimazingira.

Inaeleweka kwamba uamuzi wa kuipitia upya Sera ya Mazingira ya Zanzibar umetokana na ukweli kuwa sera iliyopo, japokuwa yo ya zamani sana, ina upungufu kwa kuwa haitoshelezi mahitaji halisi ya kuhifadhi mazingira katika namna ya kuwezesha mazingira kuiletea tija endelevu jami.

Zanzibar, nchi inayoundwa na visiwa vikiwemo viwili vikubwa na vingine kadhaa vidogo, imezungukwa na bahari kwenye pande zake zote huku bahari yenyewe ikitambaa mwambao wa Bahari ya Hindi wenye urefu wa kilomita zaidi ya 250.

Nchi hii iliyo sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imekuwa ikilazimika kuangalia upya sera yake ya mazingira kwa kuwa inakabiliwa na mfululizo wa athari za kimazingira yakiwemo haya yanayotambuliwa zama hizi kama mabadiliko ya tabianchi.

Mapitio ya sera ilipo yanafanyika huku ikithibitika pasina shaka kwamba sera iliyotungwa mwaka 2013, imepitwa na wakati kutokana na kutowezesha kutatuliwa kwa changamoto mpya zinazoibuka siku hadi siku.

Hiyo Sera ya Mazingira inayopitiwa upya, imefuatia mapitio ya mara ya kwanza ya sera iliyotungwa mwaka 1992, wakati huo serikali ikiwa ndio kwanza imeingia katika programu ya kufanya mageuzi ya kiuchumi kutokana



Othman Masoud

na kuzorota kwa tija ya sera na mifumo ya kujenga uchumi ambayo kwa sehemu kubwa ikimilikiwa na serikali peke yake.

Ni kwa kutambua ukweli huo na hususan umuhimu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kushirikisha sekta binafsi kwa ajili ya kupata mchango utakaokuwa umejumuisha mahitaji ya wakati uliopo, ndio Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, akatoa tamko rasmi kutaka mamlaka husika nchini kuhakikisha mapitio ya Sera ya Mazingira sasa yanakuwa shirikishi katika ngazi zote, kwa kuzingatia kuwa maisha ya kila siku ya wananchi yanategemea maliasili.

Makamu wa Kwanza Othman ambaye ofisi yake inashughulikia jukumu la hifadhi, uendelezaji na ulinzi wa mazingira, anasema Zanzibar inashuhudia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii yanayochagiza kuwepo kwa matumizi makubwa ya maliasili ziliopo kiasi cha kusababisha mbinyo kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka.

“Matumizi makubwa ya maliasili yanachangia kwa kiasi kikubwa kuzidi kwa mashinikizo kwenye ikolojia za baharini na nchi kavu. Hii inatosha kuwa sababu muhimu ya ulazima wa kupitiwa upya kwa Sera ya Mazingira

Mume nambari wahedi yuko wapi?

TAI, kwa miezi kadhaa amekuwa akisononeka. Kila mara anajiinamia na kuthibitisha kwamba amejawa na mawazo, lakini anasita kufunguka kueleza yanayomsibu.

Miezi zaidi ya minne, hali yake imekuwa hivyo, hata kama kuna kipindi anaonekana “kuchangamka,” na anafanya kazi zake kama kawaida, lakini akipata wasaa wa kuwa peke yake, anarudia hali yake ya kuonekana amejawa msongo wa mawazo.

Hata hivyo, Jumatatu ya wiki iliyopita, Tai baada ya kutoka Bunazi, huko Wilaya ya Missenyi, Kagera alikokwenda kutembelea wadau wake na kusikiliza kilio chao cha kuzongwa na vumbi jingi kutoka kwenye barabara inayotumiwa na magari yanayobeba miwa kuelekea Kiwanda cha Sukari cha Kagera (Kagera Sugar), hatimaye ameamua kufunguka.

Tai akiona heri afunguke yanayomsibu kwa Pambazuko kwani anaamini kwamba ama atasaidia kupatikana kwa majibu au kushirikisha wadau wengine ili dawa ya sonona ipatikane.

Bwana eh! Tai akafunguka. Akasema amejawa huzuni kwa kuwa hajamuona mume nambari wahedi wa Tanzania; Kwamba Baba Wanu ambaye ni pia ni Baba Abdul, hajamuona siku nyingi.

Kwamba Baba Abdul hajaonekana kwenye dhifa nyingi ambazo Mama Wanu ameonekana. Mbona alionekana sana siku za mwanzo – mwanzo akiwa na Mama Abdul na alitambulishwa kwenye kila hadhira aliyokuwepo!

Tai akasema alianza kusiononeka alipoalikwa kwenye dhifa ya kitaifa aliyoandaliwa Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, lakini hakumuona Baba Wanu.

Kwamba katika dhifa ile, mume nambari mbili wa Marekani, Douglas Emhoff, Baba Ella, alitambulishwa na waalikwa kwenye viwanja vya Ikulu wakashangilia kwa kumtambua.

Wakati anatambulishwa Mmarekani yule, Tai ambaye naye alikuwa mwenyewe



Rais Samia akiwa na mumewe Hafidh Ameir

– bila kuwepo Mama Tai, alisubiri kumuona Baba Wanu atambulishwe, lakini hakumuona na wala hapakuwepo taarifa yoyote kwamba labda anaumwa.

Anewe! Tai akakaa kimya, lakini akajawa mawazo kwamba iweje Baba Wanu akosekane pale, ambapo karibu kila “mtu mkubwa” wa Tanzania alikuwepo!

Tai akaikumbuka siku ya Alhamisi – Machi 30, mwaka huu ambapo Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, aliwasili Dar es Salaam, na kupokelewa na mwenyeji wake na akafurahi sana kukutana na mwanamke mwenzake ambaye ni kiongozi wa nchi, Rais Samia Suluhu Hassan.

Tai anaamini kwamba mume wa Kamala, Donald ambaye aliambatana na mkewe, alijiandaa kukutana na mume wa Rais Samia, lakini hakuna rekodi popote wanaume hao walikutana.

Sasa Tai anatamani kumuona Baba Wanu; Hafidh Ameir akiwa kwenye hadhira kwa kuambatana na mkewe, Rais Samia kila anapokwenda kwenye shughuli za serikali.

Yaani Tai anapenda kumuona Baba Wanu akisafiri kila mahali na mkewe, Rais Samia na hakika anaeleza kuwa yuko tayari kubeba mabegi ya Baba Wanu bila malipo kila anapokwenda.

Je, unapenda kuwasiliana na Tai? Mpatе kwa namba hii: 0754 020 880.

Habari

Utu umemtangulia Rugambwa - Bagonza

Na Mwandishi MAALUM

SASA ni rasmi kwamba Tanzania imepata kardinali baada ya Protase Rugambwa, Askofu Mkuu Mwamamizi wa Jimbo Kuu Katoliki Tabora kupewa hadhi hiyo juzi - Jumamosi na Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis.

Sherehe za kusimikwa hadhi ya ukardinali kwa Rugambwa zilifanyika katika wiwanja vya Mtakatifu Petro, na kushuhudiwa na dunia nzima kupitia vyombo vya habari. Maaskofu wengine 20 kutoka nchi mbalimbali walipewa hadhi hiyo.

Pambazuko limeelezwa kwamba mara baada ya Askofu Mkuu Mwamamizi Rugambwa kuvikwa joho la dhamana hiyo ndani ya Katoliki, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe, Dkt. Benson Bagonza alipewa fursa ya kuzungumza neno kuhusu maisha ya Kardinali Rugambwa.

Askofu Dkt. Bagonza, alizungumza kwa ufupi kwamba Kardinali Rugambwa amejawa utu, unyenyekezi na zaidi sana ana hekima ya kutenda haki.

“Huyu Rugambwa ambaye sasa ni Kardinali wa Kanisa Katoliki Tanzania, ni mtu ambaye hekima imemzidi kimo na utu umemtangulia mbele. Ni mnyenyekevu, lakini siyo mdhaifu. Ni binadamu mwenye nidhamu, lakini siyo muoga,” aliongeza Askofu Bagonza.

Askofu Bagonza ameonyesha njia ya ushirikiano wa makanisa kwa kuwa miongoni mwa waliohudhuria sherehe hizo kubwa kutoka kanisa jingine.

Pambazuko limeelezwa kwamba uongozi wa makao makuu wa Kanisa Katoliki, Vatican, ulifurahia uwepo wa Askofu Bagonza, akiwa kiongozi wa kanisa nje ya Katoliki na kuomba ushirikiano baina ya viongozi na waumini wa dini mbalimbali uimarishwe ili kujenga dunia yenye

Kardinali Rugambwa anakuwa Mtanzania wa tatu kupata wadhifa huu mkubwa baada ya Askofu Laurean



Papa Francis akimwekea mikono Askofu Protase Rugambwa kuwa kardinali - Picha na Riccardo De Luca wa AP

Rugambwa (sasa marehemu), Mwadhama Polycarp Pengo na sasa Kardinali Protase Rugambwa.

Kardinali Protase Rugambwa ni mzaliwa wa Karagwe, Jimbo la Kayanga, Kijiji cha Kasheshe, Parokia ya Katojo, na kwamba anatoka katika ukoo wa Abakaraza (Abarigi).

Majina yake ya kifamilia ni Protase Abakaraza. Jina la Rugambwa alipewa ikiwa ni heshima kwa Askofu Laurean Rugambwa ambaye alifanya ziara Bukoba siku aliyoziuliwa Protase.

Protase alizaliwa Mei 31, 1960 - siku ambayo Kardinali Laurean Rugambwa alikuwa na ziara ya kitume Bukoba.

Baba yake Protase akasema kwa kuwa mtoto wake alizaliwa siku ambayo Kardinali Lauren Rugambwa alikwenda Bukoba, basi mwanawe ataitwa kwa jina lake.

Taratibu za Kanisa Katoliki (RC), zinaeleza kuwa makardinali ndio washauri wakuu wa Papa na pia hutumika kumchagua kiongozi mkuu wa kanisa hilo inapotokea amefariki dunia, kuugua ugonjwa usiokuwa na matumaini ya kupona ama kupata magonjwa ya akili.

Uongozi wa gazeti la Pambazuko unamtakia majukumu mema Kardinali Rugambwa na kwamba liko tayari kushirikiana naye na kanisa lake kuhakikisha amani, maendeleo na utulivu vinatamaliza Tanzania.

Kula hovy chanzo kuugua moyo

Na Scovy MANASE

MPANGILIO mbovu wa vyakula, kutozingatia ulaji wa matunda, mbogamboga na kutofanya mazoezi, ndiyo vyanzo vikuu vya magonjwa ya moyo, Pambazuko linaeleza.

Takwimu za Wizara ya Afya Tanzania za mwaka 2022 zinaonyesha kuwepo kwa ongezeko la asilimia 9.4 kwa wagonjwa wa moyo na shinikizo la damu.

Kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita; Tanzania imerekodi wagonjwa wa magonjwa hayo kutoka milioni 2.5 mwaka 2017 hadi wagonjwa 3.4 mwaka 2022.

Waziri wa Afya wa Tanzania, Ummu Mwalimu amethibitisha hayo na kuongeza kwamba magonjwa ya moyo na shinikizo la damu yanaweza kuzuiliwa endapo mtindo wa maisha unaohudiwa sasa, kwa watu wengi utabadilika.

Akizungumza na wananchi waliohudhuria maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Hospitali ya Dar Group iliyopo Temeke, Dar es Salaam, waziri huyo alishauri pia watu kujenga utamaduni wa kutenga muda kwa ajili ya kufanya mazoezi.

Waziri Ummu pia alisema taarifa za ufuatiliaji wa magonjwa yasiyoambukiza kutoka mwaka 1980 hadi mwaka 2020 inaonesha ongezeko la magonjwa ya shinikizo la juu la damu na kisukari katika jamii kutoka asilimia moja hadi tisa kwa wagonjwa wa kisukari na kutoka asilimia tano hadi 26 kwa wagonjwa wa shinikizo la juu la damu.

“Magonjwa haya mawili ndiyo chanzo kikuu cha magonjwa ya moyo, figo pamoja na ugonjwa wa kiharusi, hivyo ongezeko hili ni tishio kwa ustawi wa afya ya jamii yetu na ndiyo sababu inatuweka hapa leo kujadili mikakati ya kukabiliana nayo...

... Matatizo haya yanaweza kuzuiliwa



Waziri Ummu Mwalimu akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani yaliyofanyika Dar es Salaam wili iliyopita -Picha na JKCI

kwa mtu mmoja mmoja na jamii yetu kwa kuchukuwa hatua, ikiwa ni pamoja na kuepuka ulaji mkubwa wa chumvi, vyakula vya mafuta na zaidi sana kuongeza ulaji wa matunda na mbogamboga,” ameingiza waziri huyo.

Amewasihi Watanzania kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi angalau dakika 150 kwa wiki na mazoezi haya siyo lazima yawe ya kukimbia – kwani hata ya kutembea ni zoezi zuri na lenye afya zaidi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mobhara Matinyi aliishukuru Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete kwa kufanya maadhimisho ya siku ya moyo duniani katika wilaya yake na kuwaomba wananchi kufanya uchunguzi wa afya zao mara kwa mara.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dkt. Angela Muhozya pia alihimiza Watanzania kubadili mitindo ya maisha, hasa kuzingatia ulaji wa kiasi wa chumvi, sukari ili kujiupusha na magonjwa ya moyo na shinikizo la damu.

Dkt. Angela alisema katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza taasisi hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi jinsi ya kuepukana na magonjwa ya moyo.

Tangazo

Ukiwa Bukoba...

Furahia Nene Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya;

Embe	Nanasi/pinacolada
Passion	Tende
Parachichi	Tikiti
Karoti	

Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.

Waziliana nazi kwa
namba hii:

0753949488





Hoja Yangu

Fedha za Lindi Sekondari ziko wapi?

Na Rashid MTAGALUKA

KAMA kuna miradi ya serikali kinayofunikwa-funikwa bila kutolewa maelezo ya kina kuhusu maendeleo yake, basi mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Lindi ni mmojawapo ambao wananchi na wadau wa elimu nchini wanahoji ukimya uliogubikwa.

Mradi wa ujenzi wa jengo la ghorofa mbili uliosimama tangu mwaka 2017, ulitokana na shule hiyo kongwe kuteketea kwa moto usiku wa kuamkia Julai 10, 2016,

Kufuatia tukio hilo, Waziri Mkuu Majaliwa Kassim Majaliwa alisema kwa namna ambavyo majengo hayo yameungua, ni vyema yakavunjwa na kujengwa upya na aliwataka viongozi mkoani Lindi kutumia nafasi hiyo kwa kujenga jengo la ghorofa ili kutumia eneo dogo kwa kujenga madarasa mengi.

Aidha, Majaliwa alimuagiza Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi kuhakikisha fedha zitakazopatikana katika harambee hiyo, ambayo mgeni rasmi alikuwa rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete hazichepushwi matumizi yake na zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Hata hivyo, inashangaza kwamba tangu 2017 mpaka leo 2023, ukifika katika sekondari hiyo utakuta msingi tu wa ghorofa lililokusudiwa na hakuna maendeleo mengine.

Taarifa zinaeleza kuwa, kwenye harambee ile iliyokusanya wadau wa elimu na viongozi mbalimbali, kiasi kilichokusanywa ni zaidi ya shilingi milioni 700 huku fedha iliyotarajiwa ikiwa ni shilingi bilioni moja.

Sasa hoja yangu ni kwamba kwanini maendeleo ya ujenzi yakomee kwenye msingi, wakati ninaamini kabisa kwamba kiasi kilichokusanywa hakijaishia kwenye hatua hiyo ya msingi pekee!

Fedha zilizokusanywa kwenye harambee ile iliyofanyika Dar es Salaam pamoja na ahadi zilizotolewa na wadau bila kusahau makato ya ndugu zangu wakulima wa korosho, kwa hatua iliyofikiwa ya ujezi, lazima zitakuwepo. Je, ziko wapi na zinafanya nini?

Pia inashangaza kwamba kwanini mpaka leo kamati ya ujenzi haitaki kutoka hadharani kuwaambia wananchi hatima ya michango yao waliojitolea ili ujenzi wa jengo la ghorofa usonge mbele? Inaelezwa kwamba katika shule hiyo kongwe ya Lindi, ikiwa kilometa chache kutoka zilipo ofisi za mkuu wa mkoa huo wanafunzi wake wanasomea uwanjani na chini ya miti kwa ukosefu wa vyumba vya madarasa huku fedha za ujenzi zikiendelea kutowekwa hadharani, hali ikoje huko maeneo ya mbali kama Nandagala, Namapwiya, Uleka na kwingineko, hali itakuwaje?

Enyi viongozi, hebu elezeni ziliko fedha zilizokusanywa na ikiwezekana zifanye kazi iliyokusudiwa. Na kama hazipo, ielezwe ziko wapi na zinafanya nini.

Kama pesa zipo, ebu viongozi tokeni hadharani muwaambie wananchi kilichokwamisha ujenzi wa Sekondari ya Lindi ilihali fedha nyingi zilipatikana kwa ajili hiyo na inashangaza kukomea kwenye msingi tu!

Mwandishi anapatikana kwa simu 0784438546 au mtagaluka@gmail.com

Habari**Bilioni 50/- kuimarisha mawasiliano**

Na Innocent MUNG'Y

Serikali ya Tanzania imesaini makubaliano ya maridhiano na watoa huduma wa mawasiliano yenye thamani ya shilingi bilioni 50 kama malipo ya matumizi ya miundombinu tangu kujengwa kwake.

Aidha, Watoa Huduma hao wameahidi pia uwekeza shilingi bilioni 32.5 katika maendeleo ya miundombinu zaidi nchini.

Tanzania imefikia makubaliano haya ya kihistoria na watoa huduma wa mawasiliano nchini katika hafla ya utiaji saini iliyofanyika Dar es Salaam mapema wiki iliyopita – Septemba 25, 2023.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na vingozi mbalimbali wa serikali wakiwemo mawaziri, makatibu wakuu na watoa huduma wa mawasiliano nchini.

Makubaliano haya yanalenga kuimarisha miundombinu ya mawasiliano, na yalijumuisha kampuni kubwa za simu za mkononi; Airtel Tanzania, Honora Tanzania (Tigo), na Vodacom Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Moses Nnauye, alisisitiza umuhimu wa kuendeleza Sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wa nchi wa Tanzania.

Waziri Nnauye alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujitolea kuweka kukuza sekta ya mawasiliano.

Nape pia alielezea dhamira ya serikali kuhakikisha huduma za mawasiliano zinawafikia wananchi wote na kuwa chachu ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Aliwapongeza viongozi wa serikali walioshiriki katika majadiliano hayo na kusisitiza umuhimu wa kuendeleza miundombinu ya mawasiliano nchi ili kufikia uchumi wa kidijitali.

Makubaliano haya ya kihistoria yalianzishwa Oktoba 4, 2011, na yalilenga kuimarisha miundombinu ya



Waziri Nape Nnauye katika hafla hiyo ya maridhiano - Picha kutoka mitandao ya wizara

mawasiliano, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa mkongo wa taifa katika maeneo ambayo hayakuwa na huduma ya mawasiliano.

Wakati wa hafla ya utiaji saini, watoa huduma wa mawasiliano walikubaliana kutoa dola milioni 20 kwa matumizi ya kipindi cha miaka mitano na kuahidi kuwekeza dola milioni 13 katika maendeleo ya miundombinu zaidi.

Hafla hiyo pia ilishuhudia kujiunga kwa Vodacom Tanzania kama mwanachama wa muungano huo, ikionyesha ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali katika kutoa huduma za mawasiliano kwa wananchi na kukuza uchumi.

Ilielezwa kwamba serikali imedhamiria inafikia lengo la kuhakikisha huduma za mawasiliano zinawafikia Watanzania wote na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa kidijitali, na inalenga kufikia asilimia 85 ya Watanzania wenye ufikiaji wa intaneti ya kasi ifikapo mwaka 2025.

Aidha, Nnauye alitoa maelekezo ya utekelezaji wa makubaliano haya na kuwasihii watoa huduma wa mawasiliano kuendelea kuwekeza katika miundombinu ili kufikia wananchi wengi zaidi.

Hafla hii ilipokelewa kwa furaha kutoka pande zote mbili na inaonyesha hatua muhimu kuelekea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano nchini Tanzania.

Bukoba Raha

... Bukoba kuna senene
... Bukoba kuna maji safi na salama

**Lakini Bukoba kuna G-smart Sauna & Steam Bath
(Bafu la kuoga kwa mvuke).**

**Ukiwa Bukoba ama unaishi, usisahau
kupata huduma G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Hakika hautajuta na ona fahari kusimulia
wengine huduma za G-smart Sauna & Steam Bath.**

**Faida za Sauna na Steam Bath ni nyingi,
lakini chache ni zifuatazo:**

- Inaboresha afya ya moyo na mishipa
- Huondoa uchovu wa mwili na misuli
- Kuondoa msongo wa mawazo (stress)
- Kuzuia magojwa ya kukakamaa kwa misuli
- Inaboresha na kuhuisha mfumo wa usingizi
- Kuondoa sumu na kufanya ngozi nyororo zaidi

**Wasiliana na G-smart and Steam Bath
walioko Barabara ya Kashozi na wapigie
simu kwa namba: 0626 265725 / 0767 291 670**

Tangazo

JIKO LAKO : FURSA YAKO

Fursa hii inawakutanisha mawaziri, wabunge, viongozi wa serikali na wajasiriamali wanawake wa Dar es Salaam kwa ajili ya kujenga mnyororo wa kukuza biashara na fursa lukuki.

Hii ni fursa adhimu ambayo kila mwenye kutamani maendeleo binafsi, familia na Tanzania yetu asipange kukosa.

Shughuli: Semina maalum; kutambulisha na kuuza bidhaa; kutoa tuzo kwa wajasiriamali mahiri wa DSM

Mahali: Ubungo Plaza, Ubungo, Dar es Salaam.

Tarehe: 14/10/2023

Muda: Kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi jioni.

**Ewe baba, dada, kaka, mjomba na shangazi, tafadhali
changia maendeleo ya familia na nchi kwa
kuwainua wamama
Karibuni sana kwa fursa lukuki.**

Tiketi

Kawaida Sh. 50,000
(VIP); Sh. 100,000.

Tafadhali wasiliana kwa namba hii ya simu
kwa maelezo zaidi: 0769 014 015

MSD yakamia kujenga viwanda zaidi

Na Mwandishi WETU

BOHARI ya Dawa (MSD) inatekeleza mkakati maalumu wa kuanzisha viwanda vya dawa na vifaatiba nchini kama njia ya kupunguza kiwango cha kuagiza vitu hivyo nje ya nchi.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, ameliambia Pambazuko kwamba mpango huo utatekelewa kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi.

Wachambuzi wa masuala ya uchumi wanausiafa mpango huo wa MSD wakisema utasaidia kuimarisha urari wa biashara kwani utapunguza bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi.

Kwa upane mwingine, wachambuzi hao walibainisha kuwa mkakati huo utasaidia nchi kupunguza matumizi ya dola za Marekani zinazotumika kuagiza bidhaa nje ya nchi, jambo ambalo sasa ni tatizo kubwa kutokana na upungufu wa sarafu hiyo inayotumika kwa kiasi kikubwa katika biashara za kimataifa.

Aidha, mpango huu umesifiwa kwa kuwa utasaidia kuendeleza sera ya nchi ya ujenzi wa viwanda jambo ambalo linakuza uchumi, kuongeza ajira na pia pato kwa mtu mmoja mmoja.

Tukai alisema kwa kuanzia MSD imeshabainisha maeneo matatu ya uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha dawa na vifaatiba nchini.

“Ili kutekeleza mpango huu, MSD itashirikiana na sekta binafsi. Tayari tumeshatangaza tenda (zabuni) kwa kuzialika kampuni ambazo zinaweza kuifanya kazi hii kwa kushirikiana nasi waombe ili tuingine kwenye ushirikiano rasmi,” alisema.

Tukai alibainisha kuwa moja ya zabuni hizo inahusu ujenzi wa kiwanda cha vifaa tiba vinavyotokana na pamba kitakachojengwa mkoani Simiyu.

Simiyu ni moja ya mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa pamba nchini huku kiasi kikubwa cha pamba hiyo ikiuzwa ghafi nje ya nchi.



Mavere Tukai

“Utafiti umeonyesha kuwa hakuna haja ya Tanzania kuagiza vifaatiba vinavyotokana na pamba, kwa sababu tunazalisha pamba ya kutosha kuweza kuzalisha vifaa hivi kwa mahitaji ya ndani,” alisema Tukai.

Alibainisha pia kuwa kupitia mradi huo, watazalisha vitambaa vitakavyotumika kutengenesa bidhaa nyingine kama vile shuka na sare za watumishi kama wauguzi na makoti ya madaktari.

Pia kuna mradi wa kuwa na kiwanda ambacho kitazalisha barakoa na glavu.

MSD pia iko mbioni kuwa na mradi mkubwa wa kiwanda kitakachojengwa Kibaha mkoani Pwani na kwamba utakaohusisha ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha dawa za aina zote.

Tukai alisema ili kuondoa muingiliano wa shughuli nyingine za MSD, wameamua kuanzisha kampuni tanzu ya MSD Medipharma Manufacturing Company Limited ambayo ndiyo itakuwa msimamizi na mshirika wa taasisi binafsi zinatazoingia ushirikiano na MSD.

Kwa mwaka ulioishia Julai 2023 Tanzania ilitumia kiasi cha dola za Marekani milioni 307 kuagiza dawa na vifaatiba nje ya nchi hivyo uwepo wa viwanda vya ndani kutasaidia kupunguza kiasi hicho cha fedha za kigeni.

Habari**NSSF yaja kivingine
kuondoa umasikini**

Na Mwandishi WETU

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umewataka Watanzania walio katika sekta isiyo rasmi; hasa machinga, kujiandaa kwani inaanazisha mpango madhubuti kuhakikisha wanashirikishwa kwenye mifumo ya hifadhi ya jamii.

Chini ya mpango wa Kitaifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Isiyo Rasmi (NISS), NSSF imesema imeandaa mfumo huo ambao utahakikisha kuwa watu wote walio katika sekta isiyo rasmi, wanafaidika kwa huduma na shughuli zinazofanywa na mfuko huo.

Mpango huu, endapo utatekelezwa kwa ufanisi, utakuwa mwanga wa kupunguza umasikini kwa kiasi kikubwa, kwani wananchi wengi wasiokuwa kwenye sekta rasmi, hawana “uhakika wa kesho yao.”

Akizungumza Dar es Salaam hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema mpango huo ni mkombozi wa uhakika kwa kupunguza umasikini unaowazingira Watanzania wengi walio katika sekta isiyo rasmi.

Sekta isiyo rasmi inahusisha watu wote wanaojihusisha na shughuli za kuiuchumi kama vile biashara ndogondogo na ujasiriamali, lakini shughuli zao hizo hazijaingizwa katika mifumo rasmi ya kiuchumi katika nchi.

Kwa mujibu wa tovuti ya world economics, ukubwa wa sekta isiyo rasmi Tanzania unakadiriwa kuwa ni asilimia 46.7 ya sekta binafsi na shughuli zake zina thamani ya dola za Marekani bilioni 78 (sawa na shilingi 195,000,000,000,000) kwa mujibu wa viwango vya kupima pato la jumla la sekta binafsi dhidi ya pato la taifa.

NISS ni skimu maalum iliyobuniwa na NSSF miaka kadhaa iliyopita, lakini haikufanya kazi vizuri.

Kwa maono Mshomba, NISS

**Masha Mshomba**

ilifanyiwa tathimini na kurekebisha ili iendane na hali halisi katika jamii na kuiwezesha NSSF kuunda mpango mzuri utakaowanufaisha walio katika sekta isiyo rasmi.

“Mpango huu utazinduliwa hivi karibuni. Mpango umeundwa baada ya kufanya tathmini na utafiti ndani na nje ya nchi na hivyo tukafanikiwa kuja na utaratibu endelevu utakaohakikisha kuwa sekta isiyo rasmi nayo inahusishwa katika mpango wa hifadhi ya jamii,” alisema Mshomba.

Mshomba alisema utafiti huo umebaini kuwa mahitaji makubwa ya watu wengi katika sekta isiyo rasmi ni fao la afya na mikopo ya kuongeza mitaji yao.

Hivyo, alisema mpango utawajumuisha watu hao katika fao la afya na mpango wa mikopo ambayo wataitumia kuimarisha mitaji yao.

Kwa mujibu wa Mshomba, mpango huu umelenga kuongeza wigo wa Watanzania wanaonufaika na hifadhi ya jamii inayotolewa na NSSF na pia ni njia ya kusaidia juhudi za serikali kupunguza umasikini wa kipato nchini.

Jinsi ya kujiunga

NSSF inaeleza kwamba katika kujiunga na mpango huo, hakutakuwa na urasimu mkubwa kwa wale watakaopenda kujiunga na mpango huu kwani watakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha taifa (NIDA) pamoja na

Endelea Uk. 16



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Habari**Meena mwenyekiti Rujat**

Na Kadama MALUNDE

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Waandishi wa Habari Vijijini (Rujat) kimemchagua Neville Meena kuwa mwenyekiti wa wake.

Katika mkutano huo uliofanyika Ukumbi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa) Kanda ya Kati jijini Dodoma jana, pia ulichagua viongozi wengine ambao ni Prosper Kwigize, katibu mkuu; Editha Majura kuwa mweka hazina na Zania Kweka akiukwaa umakamu mwenyekiti.

Pia mkutano huo uliwachagua wajumbe sita kulingana na kanda; Anne Rhobi (Pwani), Meshack Ngumba (Magharibi), Hamida Ramadhani (Kati), Musa Juma (Kaskazini), Neema Emmanuel (Ziwa) na Felix Mwakyembe (Kusini).

Akizungumza katika mkutano huo, Meena alisema kazi kubwa sasa ya chama hicho ni kupata wanachama wengi zaidi ili kujenga umoja wenye nguvu.

Kwa upande wake, Kwigize alisema lengo la chama hicho ni kuondoa utofauti wa vijijini na mijini kwani katika maeneo



Mwenyekiti wa Rujat, Neville Meena akizungumza baada ya kuchaguliwa kuongosa chama hicho. Aliyeketi ni katibu mkuu wake, Prosper Kwigize. (Picha na Kadama Malunde).

mengi ya vijijini hawapati taarifa na habari kama zinavyopatikana mijini.

“Rujat ni chama cha kipekee sana, hivi sasa kina wanachama 38. Tunataka kuandika habari za kusisimua maendeleo vijijini, tunataka kuondoa mitazamo ya kwamba hakuna haja ya kuandika habari za vijijini kwa kuamini kwamba hakuna habari za maana,” aliongeza.

Kwigize alisema Rujat imepanga kufungua tovuti ambayo itakuwa inachapisha habari mbalimbali za vijijini ili umma ufahamu yanayoendelea huko maeneo yanayosahaulika mara kwa mara.

NSSF yaja kivingine*Inatoka Uk. 14*

simu iliyosajiliwa kwani huduma nyingi zitatolewa kupitia simu za mikononi.

Kiwango cha chini cha mchango kwa mwananchama ni shilingi 20,000, ambacho kitawasilishwa kupitia simu ya mkononi au kupitia mawakala wa benki na mitandao ya simu za mikononi.

Wanufaika

Mtu yeyote aliye katika sekta isiyo rasmi kama kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji mdogo wa madini, mfanyabiashara ndogondogo, mama na baba lishe, watakuwa na haki ya kijiunga na mpango huu.

Aidha, watu ambao walilipwa mafao

yao baada ya kuachishwa kazi, wanaweza kujiunga na mpango huu miezi 18 baada ya ajira zao kukoma.

Mafao

Mwananchama wa mpango huu anaweza kupata mafao ya uzeeni ya pesheni, mafao ya matibabu na mafao ya kifo.

Pia kutakuwa na mafao ya vitu badala ya fedha taslim ambayo yatolewa kulingana na shughuli, biashara au sekta aliyomo mwananchama.

Mafao haya yatahusisha mashine au vifaa vya kazi na yatatolewa kulingana na muda wa michango ya mchangiaji.

Rais Ruto acharuka, hataki wavamizi

Na Mwandishi WETU,
Nairobi

LIMEKUWA tatizo la muda mrefu kwa baadhi ya raia wa Kenya, kama ilivyo kwa wenzao wa Uganda na Tanzania, kuvamia maeneo ya hifadhi na hata vyanzo vya maji.

Uvamizi huu, siyo kwamba unavuruga vyanzo vya maji na maisha ya viumbe anuai, lakini pia unaharibu ikolojia ya mazingira katika maeneo husika.

Sasa kwa kutambua hilo, na wananchi hao kukaidi kuondoka maeneo hayo, hatimaye Rais wa Kenya Dkt. William Ruto ameapa kuwaondoa haraka iwezekanavyo.

Rais Ruto alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wananchi mjini Narok, nje kidogo ya Jiji la Nairobi wakati wa kusanyiko la mazishi.

Kiongozi huyo alisema wakati wa kuondoka kwa nguvu wavamizi wa maeneo mahsusi, umefika na kwamba serikali haitakuwa na mzaha katika zoezi la kuwaondosha wakaidi.

“Naagiza watu wote, hawa maskwota wote waliokita kambi katika misitu iliyohifadhiwa, kuondoka mara moja kabla ya kukabiliwa na sheria,” alisema kwa lugha yenye sauti ya ukali.

Rais Ruto aliwataka watu wote waliovamia misitu, hasa Msitu wa Mau, kuondoka mara moja kabla “mkono wa sheria” haujawafikia.

Alisema wote watakojifanya kuwa “vichwa ngumu,” nguvu ya dola itatumika kuwaondoa na hakutakuwa na mjadala kwa lolote.

Rais Ruto pia alisema kuwa serikali iko katika hatua za mwisho za kuzungushia uzio misitu yote muhimu yenye chemicheni ya maji.

“Tutaweka uzio kuzunguka minara yote ya maji nchini ili kuilinda dhidi ya



Rais Ruto

kuvamiwa. Hii ndiyo sababu ninawaomba wale ambao wamevamia kuhama mara moja,” aliongeza Rais Ruto.

Msitu wa Mau ni muhimu zaidi kati ya misitu mingine kumi inayotegemewa na idadi kubwa ya Wakenya kuwa vyanzo vikuu vya maji asili ya Kenya.

Hata hivyo, kumekuwa na vuta nikuvute kwa miaka mingi kutokana na ‘maskwota’ waliovamia misitu hiyo kugeuka waharibifu wa vyanzo vya maji na kukata miti kwa ajili ya matumizi ya ardhi.

Kufurushwa kwa wavamizi hao kutoka maeneo ya vyanzo vya maji kulianza mwaka wa 2005 chini ya utawala wa Rais Mwai Kibaki, lakini hawakuweza kuondoka, licha ya serikali kubatilisha hati miliki zote katika eneo la Mau.

Msitu wa Mau ni kati ya maeneo makubwa zaidi ya vyanzo vya maji katika eneo la Afrika Mashariki linalofunika ekari 675,000 katika Bonde la Ufa.

Kwa sasa Msitu wa Mau unasimamiwa na Shirika la Misitu nchini Kenya, KFS.

Hatua kama hii ya kuwafukuza maskwota kutoka misitu na ardhi za hifadhi, imekumbwa na mapingamizi kutoka kwa waanchi, ambao wanadai maeneo hayo ni mali yao ya asili.

Riwaya**Tetemeko la ndumba - 4**

Mtunzi: Innocent N. ZAGALLO

BAADA ya kufanya hiki na kile katika maandalizi hayo, hatimaye alijipweteka sofani na kupumua kwa nguvu. Akaisumbua akili yake kufikiri ni kipi cha muhimu ambacho huenda amekisahau. Dakika mbili, tatu alizotulia zilitosha kumfanya aamini kuwa hakukuwa na kitu chochote kingine kilicho muhimu katika safari hiyo ambacho amekisahau.

Ndipo akamwita mkewe na kumwonya, “Uwe mwangalifu na vijizi vinavyozurura usiku kucha kwenye majumba ya watu. Sitarajii kuchukua zaidi ya siku tatu kule Dar. Na kama sitarudi na Shaka, basi nitahakikisha kuwa namwacha katika mazingira mazuri ya kurudi uraiiani ndani ya siku saba tu. Lazima kifanyike kitu.”

“We Baba Shaka!” mkewe alisema huku akijishika shavu kwa mshangao. Kisha akaongeza, “Una hakika na hayo unayon’ambia?”

“Naamini Mungu atanisaidia. Najua mwan’etu, Shaka anapata pesa kwa njia ambazo dini mbili kubwa duniani, Uislamu na Ukristo haziafikiani nazo. Ni mwizi! Tuseme ni jambazi! Ukweli ndio huo! Lakini sisi tunatakiwa kujali kuwa ni mwan’etu. Ni damu yetu. Ni mwanangu, ni mwanao! Umenielewa?”

“Nimekuelewa kidogo.”

“Siyo unielewe kidogo, unielewe sana!” Mzee Songoro alifoka. “Yule ni mtoto wetu! Tunapaswa kumwkoa. Pesa alizokuwa anatutumia ndizo zimefanikisha kupata hii nyumba. Yeye halijui hilo! Hivi unadhani koo na familia mbalimbali zinashamiri vipi mitaani na kuonekana kuwa wameendelea? Unadhanai watu wanaendelea kilahali tu? Na siku hizi nd’o mambo yamezidi hasa kwa hao wanaowau wanadamu wenzetu; albino....dah...”

“Sijui dunia inakwenda wapi... lakini tuachane na hao washenzi was’jali uhai wa wanadamu wenzao,

*Uganga*

mimi nazungumzia mapenzi yangu kwa mwanangu. Yeye hachuni ngozi, hamtafuti albino, hamtafuti mtu mwenye upara wa asili...mwanangu ni tofauti mama Shaka! Yeye anasaka pesa kivyake! Akikuotea, unaye!”

Mzee Songoro akasitisha kuzungumza, akahema kwa nguvu na kumtazama mkewe kwa jicho kali, jicho lililomtisha mama Shaka.

“Basi, baba Shaka,” Mama Shaka alimkatiza. “Nimekuelewa Baba Shaka. Nenda...nenda ukamwoko mwan’etu. Nenda!”

Treni ya abiria iliondoka mjini Kigoma saa 11.00 jioni. Siku ya pili Mzee Songoro alikunywa chai mjini Tabora saa 12.30 alfajiri. Mchana huo akasota ndani ya treni hiyo hadi jioni alipotinga ndani ya Mji wa Dodoma. Siku ya tatu, saa nne asubuhi aliingia jijini Dar es Salaam.

Hakuwa mgeni wa jiji hilo. Mara kadhaa kwa miaka kadha wa kadha iliyopita alikuwa akifika katika jiji hilo kwa shughuli zake binafsi au kwa kutembelea ndugu, jamaa na marafiki.

Kwa hali hiyo, hakupata shida kutafuta usafiri wa kumfikisha Magomeni Mapipa. Kwanza alitembea taratibu hadi eneo la Mnazi Mmoja katika kituo cha ‘Baridi’ na hapo alisubiri kwa dakika chache tu kabla hajapata usafiri wa daladala.

Itaendelea wiki ijayo...

Uchambuzi

Z'Bar yazinduka kulinda mazingira

Inatoka Uk. 4

ili kwenda sambamba na kukabiliana na changamoto za kimazingira,” alisema kwenye mkutano maalum wa kuzindua mpango wa kupitia sera ya Mazingira ya Zanzibar, ulioandaliwa na asasi isiyo ya kiserikali iitwayo Climate Action Network yenye makao makuu yake jijini Dar es Salaam.

Katika ufunguzi wa mkutano huo uliofanyika Hoteli ya Golden Tulip, Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza alisema wakati huu ndio hasa unaopasa kuielekeza nchi na taifa, katika maendeleo endelevu, yanayozingatia matumizi bora ya maliasili za baharini na nchi kavu.

“Kwa ajili ya kufikia kwenye azma hiyo, ni vyema mchakato wetu wa kupata sera mpya ya mazingira uwe shirikishi katika ngazi zote, ili pia kupata maoni kamili ya wadau kuhusu mambo muhimu na ya msingi yanayofaa kuzingatiwa kwenye sera inayozamiwa kutungwa pamoja na kuelewa ni upi wajibu wa wadau katika kuhakikisha utekelezaji wake,” alisema.

Othman anabainisha kuwa miaka 10 imepita tangu kuzinduliwa kwa Sera ya Mazingira baada ya kuirekebisha ya kwanza ya mwaka 1992 na kumekuwa na uamuzi mbalimbali wa kitaifa, kikanda na katika ngazi ya kimataifa yanayoelekeza Zanzibar kufikia lengo la Maendeleo Endelevu, yakiwa ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050.

Pia ikihusisha Mpango wa Maendeleo wa 2021-2026; Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani (Zanzibar Green Legacy Programme), kwa azma pia ya kusimamia utekelezaji wa Mikataba, Maazimio na Makubaliano ya Kimataifa juu ya Usimamizi wa Mazingira na pia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia na au imesaini pamoja na kuwepo sera nyengine mpya za kisekta kama ya karibuni kabisa ya Uchumi wa Buluu.



Kima wekundu wanaopatikana Msitu wa Jozani, Zanzibar

Ufafanuzi huo wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar unamaanisha kuwa Zanzibar katika hali yake ya asili ilikuwa na mazingira mazuri, yenye fukwe za kupendeza, bahari iliyojaa raslimali za aina tofauti, udongo wenye rutuba, miti na wanyama wa aina kwa aina, mambo yaliyochangia kuipa nchi nafasi ya kupata maendeleo yaliyopo.

Maendeleo yaliyofikiwa ni pamoja na ongezeko la kutambuliwa kimataifa kwa maeneo oevu yanayohitaji kutunzwa kwa umakini ili uasili wake wa kimaumbile uendeleo kubakia. Hayo ukiacha yaliyozoeleka ya Hifadhi ya Jozani wanakoishi tumbili weupe, ni pamoja na eneo la Ghuba ya Menai inayoanzia Kusini mwa Kisiwa cha Unguja ikijumisha eneo la bahari wanapoishi pomboo (Dolphin), na Hifadhi ya Kibayolajia Anuwai ya Chwaka.

Xxx

Lakini sasa, anatahadharisha kuwa hali imeanza kubadilika na kuwepo vikwazo vingi vya kimazingira vinavyotishia kufikiwa kwa maendeleo endelevu na yanayozingatia malengo endelevu kwa mujibu wa mtazamo wa miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

“Hali halisi ya manadiliko ya tabianchi ni tishio kubwa kwa mustakabali wa maendeleo endelevu ya Zanzibar na Taifa kwa upana wake.

HAYA TUPIME MOYO



Daktari bingwa wa magonjwa ya moyo wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Salehe Mwinchete akipima jinsi moyo wa mteja wake unavyofanya kazi. Zaidi ya watu 689 walifanyiwa uchunguzi wa afya zao katika banda la JKCI wakati wa maonyesho ya sita ya kitaifa ya teknolojia ya madini yaliyomalizika juzi – Septemba 30 mjini Geita. (Picha na JKCI)

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

